Washington State Department of Social & Health Services

Mpango wa Uwajibikaji wa Kibinafsi (IRP)

Individual Responsibility Plan (IRP)

KITAMBULISHO CHA JAS	NAMBA YA KESI
KITAMBULISHO CHA MTEJA	

Mpango wa Uwajibikaji wa Kibinafsi wa WorkFirst wa _____

Ninafahamu:

- Ninahitajika kufanya kazi, kutafuta kazi, au kujiandaa kwa kazi.
- Lazima nishiriki katika shughuli zinazohitajika. Nikikosa, nitapokea adhabu isipokuwa kama ninaweza kudhibitisha kwamba nilikuwa na sababu nzuri. Hii inaitwa kuwa katika hali ya kuwekewa vikwazo ya WorkFirst.
  - Nikiwekewa vikwazo, hii inamaanisha:
    - Ruzuku yangu itapunguzwa kwa asilimia 40 au hisa ya mtu mmoja, yoyote ambayo ni kubwa zaidi, AU:
    - Ruzuku yangu itafungwa ikiwa sitashiriki katika kesi yangu ya kutotii uajiri au mkutano wa ziara ya nyumbani/mbadala.
  - Ikiwa ruzuku yangu imepunguzwa kutokana na kikwazo cha WorkFirst:
    - Lazima nifuate IRP yangu kwa wiki nne mfululizo ili nitoke kwa vikwazo.
    - Mara tu ninapofanya kinachostahili kwa wiki nne mfululizo, adhabu yangu ya kikwazo itaondolewa kuanzia mwezi wa kwanza kufuatia wiki zangu nne za kuhusika.
    - Huenda kesi yangu ikafungwa ikiwa nitabaki nikiwa nimewekewa vikwazo kwa miezi miwili mfululizo.
  - Ikiwa kesi yangu imefungwa kutokana na kikazwo cha WorkFirst:
    - Nitahitajika kuomba tena na nitahitajika nihusike kwa wiki nne mfululizo kabla ya kupokea pesa.
    - Huenda nikapigwa marufuku kabisa dhidi ya kupokea TANF/SFA, ikiwa kesi yangu imefungwa mara tatu (3) au zaidi.
- Kesi yangu imefungwa mara _____ kwa sababu ya vikwazo vya WorkFirst tangu Machi 1, 2007.
- Ni lazima nishirikiane na Divisheni ya Kuwasaidia Watoto ninapokuwa nikipokea faida za TANF/SFA isipokuwa kama ninasababu nzuri ya kutoshirikiana. Ukusanyaji mzuri wa usaidizi wa watoto unaweza kunisaidia kuondoa hitaji langu la usaidizi wa kifedha.
- Ninaweza kupata miezi 60 ya faida za kifedha za TANF/SFA maishani mwangu isipokuwa kama ninafaa nyongeza.
- Nimetumia miezi _____ ya faida za kifedha.
- Ninahitajika kufanya kazi, kutafuta kazi, au kujiandaa kwa kazi. Ikiwa siwezi kuhudhuria shughuli iliyopangiwa, nitamwita mtu huyo kwenye namba iliyoorodheshwa hapo chini.
- Lazima nifanye shughuli zifuatazo kwa jumla ya muda kila wiki uliyoelezwa hapo chini:

Ikiwa kuna sababu nzuri ya kutofuata mpango wangu, ni lazima niwasiliane na nifanyekazi na Mtaalamu/Mfanyakazi wa Jamii wa Mpango wa WorkFirst haraka iwezekanavyo. Baadhi ya mifano ya sababu nzuri ni pamoja na:

- Nilikosa miadi kwa sababu ya ugonjwa au ukosefu usiotarajiwa wa huduma ya mtoto wangu au usafiri;
- Nina hali ya dharura (kimwili, kiakili, au kimhemko);
- Mini ni mhasiriwa wa mzozo wa familia;
- Siwezi kupata huduma ya watoto inayofaa au ninayoweza kumudu katika eneo langu kwa watoto chini ya umri wa miaka 13;
- Nina shida ya sasa ya kisheria;
- Nina ulemavu au hali zingine na zimenifanya nisiweze kutimiza mahitaji ya mpango huu; au
- Mimi ni mtu mzima ambaye ana ulemavu mkali wa kurithi;
- Ninahitajika nyumbani ili kumhudumia mtoto aliye na mahitaji maalum au mtu mwingine mzima aliye na ulemavu;
- Nina umri wa miaka 55 na ninamlea mtoto na mimi siye mzazi wa mtoto huyo; au
- Ninaomba SSI na msaidizi wa DSHS.

Ikiwa sikubaliani na mpango huu, nina haki ya kuomba uhakiki wa kesi na/au kusikilizwa. Ili kuomba kusikilizwa, lazima niwasiliane na Ofisi yangu ya Huduma za Jamii au Office of Administrative Hearings, DSHS, PO Box 42489, Olympia WA 98504-2489, kati ya siku 90 ya tarehe ambayo msimamizi wangu wa kesi alitia saini hapo chini. Nimepewa nakala ya Mpango wangu wa Uwajibikaji wa Kibinafsi. Wakati wa usikilizaji, nina haki ya kujiwakilisha, kuwakilishwa na wakili au mtu mwingine ninayemchagua. Huenda nikaweza kupata ushauri wa kisheria usiokuwa na malipo au uwakilishi kwa kuwasiliana Ushauri Ulioratibiwa wa Elimu ya Sheria na Marejeo (CLEAR) kwa:

- Kutembelea tovuti yao http://nwjustice.org/get-legal-help;
- Kupiga simu kwa 1-888-201-1014 kama niko chini ya umri wa miaka 60, au
- Kupiga simu kwa 1-888-387-7111 kama nina umri wa miaka 60 au zaidi

CASE MANAGER'S SIGNATURE	DATE	SAINI YANGU	TAREHE

KITAMBULISHO CHA JAS	NAMBA YA KESI	KITAMBULISHO CHA MTEJA

MAHITAJI YA KISIRI

Ninaweza kupata huduma ya usaidizi ili kunisaidia kuendelea kazini, kutunza kazi yangu, kukubali kazi, kutafuta kazi, au kufuata mpango wangu. Ikiwa sikubaliani na uamuzi kuhusu huduma ya usaidizi, ninaweza kuuliza uhakiki wa kesi na/au kusikilizwa. Nitauliza Mtaalamu/Mfanyakazi wangu wa Jamii wa Mpango wa WorkFirst ikiwa ninahitaji huduma za usaidizi kama:

- Ukarabati wa gari
- Mavazi
- Ushauri
- Nepi
- Gharama za elimu
- Usafi wa kibinafsi
- Leseni/ada
- Kukatwa nywele
- Vyeti vya basi
- Posho ya usafiri
- Vifaa vya kazi
- Kupanga uzazi

Nikiwa bado nimewekewa vikwanzo, siwezi kupata huduma ya usaidizi (kama vile fedha za mavazi ya kikazi au usafiri) hadi nianze kufuata IRP yangu.

Ninaelewa kwamba, nikikataa kushirikiana na Divisheni ya Kuwasaidia Watoto (DCS) bila sababu nzuri, ruzuku yangu inaweza kupunguzwa. Sababu nzuri ni pamoja na tishio la kudhuriwa kwa watoto wangu au mimi. Ninaelewa kwamba nikiwa bado ninapata usaidizi wa TANF, usaidizi wowote wa mtoto uliyokusanywa huwekwa ili kulipa serikali.

Ninapoacha kupokea TANF/SFA, DCS itakusanya usaidizi wa mtoto na kunitumia isipokuwa kama nimewauliza wakomeshe. Ninaelewa huduma za usaidizi, vikwazo, na usaidizi kwa watoto.

CASE MANAGER'S SIGNATURE	DATE	SAINI YANGU	TAREHE